TANGAZO LA SERIKALI NA. 82 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA SAKURA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya kupanga eneo la Sakura ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya Jumla na ya Kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira -nukta 488005MS, 9380657KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira - nukta 488780MS, 9380458KZ; kwa umbali wa kilomita 0.784, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira –nukta 488213MS, 9379199KZ; kwa umbali wa kilomita 1.376, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenye majira - nukta 487618MS, 9379164KZ; kwa umbali wa kilomita 0.581, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba 487451MS, 9379749KZ; kwa umbali wa kilomita 0.609, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira -nukta 487735MS, 9379749KZ; kwa umbali wa kilomita 0.292, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira - nukta 487735MS, 9379820KZ; kwa umbali wa kilomita 895.35.hadi ulipoanzia''

Dodoma
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*